TANGAZO LA SERIKALI NA. 2 LIMETOLEWA TAREHE 4/1/2019

SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
(SURA. NA 272)

# AMRI

*(Imetolewa kwa mujibu wa kifungu Na.28 (d))*

AMRI YA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA SHINYANGA ("SHINYANGA WSSA") (YA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA), 2019

Kichwa cha Amri

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga ("Shinyanga WSSA") (ya Kurekebisha Bei za Huduma za Maji safi na Usafi wa Mazingira), ya Mwaka 2018.

Tarehe ya kuanza

2. Amri hii itaanza kutekelezwa rasmi kuanzia tarehe 1 Februari 2019.

Marekebisho ya bei

3. Bei za majisafi na usafi wa mazingira za Shinyanga WSSA zinarekebishwa kulingana na Jedwali la Kwanza katika Amri hii.

Masharti

4. Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti yafuatayo-

(a) ifikapo tarehe 30 Aprili 2019 au kabla, Shinyanga WSSA itawasilisha EWURA Mpango wake wa Kibiashara uliopitiwa upya kwa

kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Amri hii;

(b) Shinyanga WSSA, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Amri hii;

(c) Shinyanga WSSA itafikia viashiria vya utendaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Tatu la Amri hii;

(d) Shinyanga WSSA, kwa kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Amri ya bei na kila kifungu cha gharama katika mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa;

(e) Shinyanga WSSA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Shinyanga WSSA ikilinganishwa na Mamlaka nyingine za majisafi na Usafi wa Mazingira na uboreshaji wa huduma zake. Pia EWURA itazingatia tathmini hii katika kufanya maamuzi ya maombi yote yatakayowasilishwa na Shinyanga WSSA katika siku zijazo.

Kutenguliwa kwa Amri

5. Amri hii inatengua matumizi ya Amri Na. 2015-00 katika maeneo yanayohudumiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga ('Shinyanga WSSA').

MAJEDWALI

JEDWALI LA KWANZA

BEI, ADA NA TOZO ZILIZOIDHINISHWA

Jedwali Namba 1(a): Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi/ Mita ya Ujazo)

| Kundi la Wateja | Matumizi ($m^3$ | Bei za Sasa | Bei Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Majumbani | 0-5 $m^3$ | 1,100 | 1,360 | 1,420 | 1,490 |
| | >5 $m^3$ | 1,280 | 1,580 | 1,650 | 1,740 |
| Taasisi | | 2,070 | 2,550 | 2,640 | 2,760 |
| Biashara | | 2,110 | 2,600 | 2,690 | 2,790 |
| Viwanda | | 2,160 | 2,640 | 2,700 | 2,850 |
| Magati | | 1,000 | 1,250 | 1,250 | 1,500 |
| Viwanda vya Vinywaji | | 3,170 | 3,500 | 3,650 | 3,750 |
| Wastani wa Ulinganisho | | 1,488 | 1,835 | 1,923 | 2,014 |

Jedwali Namba 1(b): Tozo ya Huduma ya Sasa na Iliyoidhinishwa (Shilingi/Mwezi)

| Kundi la Wateja | Tozo ya Sasa | Tozo Iliyoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Majumbani | 2,500 | Wateja wa Shinyanga WSSA Hawatozwa Tozo ya Huduma | | |
| Taasisi | 4,500 | | | |
| Biashara | 4,500 | | | |
| Viwanda | 10,000 | | | |
| Viwanda vya Vinywaji | 10,000 | | | |

Jedwali Namba 1(c): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Maunganisho ya Maji Safi (Shilingi/Maunganisho)

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Iliyoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Wateja Wapya Wote | Asilimia ishirini (20%) ya gharama za maunganisho kama inavyojieleza katika sehemu ya 24 ya Kanuni za Maji za mwaka 2013 | Asilimia ishirini (20%) ya gharama za maunganisho kama inavyojieleza katika sehemu ya 24 ya Kanuni za Maji za mwaka 2013 | | |

Jedwali Namba 1(d): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Kurejeshewa Huduma ya Maji Baada ya Kukatiwa (Shilingi/Kurejeshewa Huduma)

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Majumbani | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 |
| Taasisi | 20,000 | 20,000 | 20,000 | 20,000 |
| Biashara | 20,000 | 20,000 | 20,000 | 20,000 |
| Viwanda | 20,000 | 20,000 | 20,000 | 20,000 |
| Viwanda vya Vinywaji | 50,000 | 50,000 | 50,000 | 50,000 |

JEDWALI LA PILI

MIRADI ITAKAYOTOKELEZWA – MILIONI ZA SHILINGI

| Maelezo ya Kazi zitakazofanyika | | | | Mwisho wa Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | |
| Ukarabati na Mabadilisho | | | | |
| Kubadili mabomba ya Platiki urefu wa Km 6 na mabomba ya Chuma urefu wa Km 1.7 | 217.00 | 225.00 | 234.00 | 30 Juni 2021 |

TANGAZO LA SERILKALI NA. 2 *(linaendelea)*

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kukarabati tangi la maji la Chibe | 15.00 | 24.00 | 32.00 | 30 Juni 2021 |
| Kubadili vali dhibiti 6 | 114.00 | 114.00 | 114.00 | 30 Juni 2021 |
| Kubadili vali kipepeo 20 | 167.00 | 171.00 | 172.00 | 30 Juni 2021 |
| Kubadili vali elea 12 | 4.00 | 10.00 | 10.00 | 30 Juni 2021 |
| Kubadili dira za maji 8100 kwa wateja wa majumbani | 149.71 | 252.27 | 268.51 | 30 Juni 2021 |
| Kununua na kufunga dira za maji mengi 8 | 96 | | | 30 Juni 2019 |
| Ukarabati wa majengo ya ofisi | 18 | 22.4 | 23.09 | 30 Juni 2021 |
| Kununua tarakirishi 14 | 10 | 8 | 10 | 30 Juni 2021 |
| Kununua Magari mawili | 86.97 | 90.79 | 94.7 | 30 Juni 2021 |
| Jumla-Ukarabati na Mabadilisho | 877.68 | 917.46 | 958.3 | 30 Juni 2021 |
| | | | | 30 Juni 2021 |
| Uwekezaji Mpya | | | | |
| Kununua jenereta moja | 10.00 | 10.00 | 10.00 | 30 Juni 2021 |
| Kununua mashine moja ya kuunga vyuma | 10.00 | 10.00 | 10.00 | 30 Juni 2021 |
| Kununua kikatio cha mabomba kimoja | 10.00 | 15.00 | 15.00 | 30 Juni 2021 |
| Jumla Uwekezaji Mpya | 30.00 | 35.00 | 35.00 | |
| Jumla ya Gharama za Uwekezaji | 907.68 | 952.46 | 993.30 | |

TANGAZO LA SERILKALI NA. 2 *(linaendelea)*

JEDWALI LA TATU

VIASHIRIA VYA UTENDAJI (2018/19 – 2020/21)

| Maelezo | Uniti | Lengo la Utendaji | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Idadi ya wateja wapya wa maji safi | Na | 1200 | 1200 | 1200 |
| Kiwango cha upotevu wa maji | % | 18 | 18 | 18 |
| Wateja wenye Dira | % | 100 | 100 | 100 |
| Kiwango cha ufanisi katika ukusanyaji wa mapato | % | 90 | 90 | 90 |

Dodoma,
...................., 2018

NZINYANGWA E. MCHANY
*Mkurugenzi Mkuu*